



MTANDAO SALAMA KWA WANAWAKE





PENDO

LULU

AMANI

NYANYA

BAHATI

DADA WATATU - LULU, PENDO NA AMANI - WAKIENDA NYUMBANI
KWA NYANYA KUMTEMBELEA



KARIBUNI! KARIBUNI!
NIMEFURAHI
KUWAONA.



SALAMA, NAENDELEA SALAMA
NYANYA, NINAJARIBU TU BAHATI
YANGU KWENYE SIASA

EH HEH...
UNAENDELEAJE?

VIZURI SANA!
UNAGOMBEA
NAFASI IPI?

LIGAVANA!

AHAA, HIVYO NI VIZURI!

LAKINI UNAFHAMU SIO RAHISI KUWA KWENYE UMMA, WATU WANAZUA CHECHE ZA MANENO KAMA "HANA MUME, NDIO MAANA YEYE ANA MAJUNGU. HANA WATOTO, NDIO SABABU HANA KITU BORA CHA KUFANYA ZAIDI YA KUWAAMBIA WANALUME CHA KUFANYA! MBONA MANENO KAMA HAYA HAYAELEKEZEWI WANALUME?!

HUWA SIJUI NIVALIE VIPI. NIKIPENDEZA, WANATENGENEZA ORODHA YA "WAGOMBEA LGAVANA WAREMBO ZAIDI". NISIPOPENDEZA, WANANIKEJELI! HADI TIMU YANGU YA KAMPENI INANISHAURI KWAMBA ITANILAZIMU KUUBADILISHA MUONEKANO WANGU WA KIKE. #MAMA MAHUSTLER #WAKILIBABE



yuko.co.ke • Follow



936 likes

yuko.co.ke Mkali
Amani opts for feminine look

YUKO

Kenya News → Politics

POLITICS LOCAL NEWS

Governor-hopeful tries luck in politics where luck in love has failed

55 minutes ago • read comments • by Sana Malembe



@yukopost @yuko.co.ke Mar 8

#mama mahustler scolds the opposition like they were the children she never had

POLE AMANI. UNAFHAMU SIKU ZOTE WATU WANASEMA WANACHOTAKA KUKISEMA. USIWAJALI. WEWE FANYA KILE UNACHOHITAJI KUKIFANYA KUIFANYA KAUNTI HII KUWA BORA. UNaweza LIKAFANYA BORA KAMA HAO WANALUME, AU HATA KUWAPIKU NA UBORA. WAKATI MWINGINE TUNALAZIMIKA KUJIFANYA SISI SIO BORA KADRI YA KIWANGO CHETU ILI TUSIWATIE HOFU WATU WALIO KARIBU NASI.



MBONA UNAZIJIBU?

NAAM, SIKU HIZI HUWA NAJIBU KEJELI.


NYANYA, NI HALI YA KUWAKARIPIA KWA KUZUA CHECHE ZA MANENO.

KUMBE!

INANILAZIMU PIA KUWAZUIA WATU AU KUONDOA MACHAPISHO AMBAYO NI YA KUCHUKIZA WAKATI WOTE. INACHOSHA.


UNAWAZUIA AU KUYAONDOA VIPI?

NYANYA, WATU HUANDIKA VITU MTANDAONI LAKINI UNaweza KUBADILISHA MIPANGILIO YAKO ILI KUIDHINISHA KILICHOCHAPISHWA KWENYE UKURASA WAKO KABLA HAKIJACHAPISHWA, AU KUCHAGUA UNACHOSHIRIKI NA UMMA NA KILE UNACHOSHIRIKI NA WATU UNAOWAAMINI.



NILIPOANZA BIASHARA YANGU YA MTANDAONI, NILIDHANIA YA KUWA INGEKUWA RAHISI KULIKO DUKA LA KAWAIDA KWA SABABU ISINGENIGHARIMU KULIPA ADA YA KODI N.K LAKINI NILIGUNDUA ILIKUWA NI CHANGAMOTO KATIKA NJIA NYINGINEZO. UNAGHARAMIKA SANA UKIJARIBU KUTANGAZA BIDHAA ZAKO. UNAJIBU MASWALI MENGI SANA AMBAYO HAYAISHII KUKUWA MAUZO YOYOTE. WATU WANAKUNYANYASA BURE, WANAKUITA #MKONDE, #SURAMBAYA, WANAILIZA KWA NINI UNAFANYA KAZI ILHALI UNA MUME...

YANI, INANIFANYA NIHISI KUTOFANYA KAZI NA KUKAA TU NYUMBANI WAKATI MWINGINE. INAWEZA IKAKUKATIZA TAMAA!



LO! HUU MTANDAO
UNAONEKANI KANA
KWAMBA SIO MAHALA
PAZURI PA KUFANYA
BIASHARA. LAKINI HATA
KATIKA MAISHA HALISI,
WATU WATATOA MAONI
KILA WAKATI NA LAZIMA
UKOMAE. ... PENDO,
LAKINI MBOHA
UMEKUWA KIMYA SANA?




NILIKUWA NA TUKIO BAYA NYANYA. MPENZI
NILIYEACHANA NAYE ALICHAPISHA PICHA
ZANGU ZA UTUPE MTANDAONI.

ETI NINI? UMEANZA TU KWENDA
KWENYE MTANDAO NA TAYARI
MAMBO MABAYA YANAKUKUTA!

NILIJIPIGA PICHA
NIKIWA UCHI NA
KUMTUMIA KWA
SABABU
NILIMPENDE
NA NILITAKA
ANIPENDE. LAKINI
TULIGOMBANA NA
AKAZICHAPISHA
KOTE!




zuzu
MALAYA
Poko
feki
mnene
mnyonge
sura
mbaya
kisura
fala



LAKINI ANGALAU AMANI
ALIKUWA AMENISHAURI
YA KWAMBA IWAPO
NITAWAHI KUCHUKUA
ICHA ZA UTUPLU,
NISISHIRIKI
USO WANGU.


UNAMSHAURI DADA
YAKO JINSI YA KUPIGA
PICHA ZA UTUPLU?!!

PICHA SALAMA ZA
UTUPLU NYANYA.
HAKUNA
ATAKAYEWEZA
KUMTAMBUA PASI



NA KUSHIRIKI USO WAKE! JAPO
INATIA AIBU KUWA NI MIMI, ANGALAU
NI VIGUMU KUTAMBUA KUWA NI MIMI.
WOI, WOI, WOI,
WASICHANA.
KUWA
MWANAMKE

NYAKATI HIZI! NA KWENYE MTANDAO? HEBU NISALIE KUWA NA
SIMU YANGU YA KAWAIDA TU. BAHATI HUNITOLEA PESA, NA
KUNITUMIA JUMBE ZANGU. NINI KINGINE ZAIDI NINACHOHITAJI?



BAHATI, UNASEMAJE
KUHUSU TAARIFA
HIZI ZOTE?

YAANI, SIKUJUA JINSI ILIVYOKUWA
VIGUMU KWA WANAWAKE MTANDAONI
WAKATI NIMEKUWA NIKITOA CHECHE ZA
MANENO HAYO NA MARAFIKI ZANGU.

LAKINI MBONA
LIFANYE HIVYO?

SIJUI.
ILIONEKANA
KUWA JAMBO
ZURI. LAKINI
SASA NAONA
INAWEZA
KULUMIZA.



JE! UKATILI DHIDI YA WANAWAKE MTANDAONI (UDYWM) AU UHALIFU WA KIJINSIA MTANDAONI NI NINI?

- ▶ **UHALIFU WA KIMTANDAO** NI SHUGHULI ZA UHALIFU AMBAZO AIDHA HULENGA AU KUTUMIA KOMPYUTA, MTANDAO WA KOMPYUTA AU KIFAA KILICHOLINGANISHWA KWENYE MTANDAO.
- ▶ **UKATILI WA KIJINSIA** NI UNYANYASAJI UNAOELEKEZWA MWANAMKE KWA SABABU YEYE NI MWANAMKE AU AMBAO UNAATHIRI WANAWAKE KWA KIASI KIKUBWA.
- ▶ **UKATILI DHIDI YA WANAWAKE MTANDAONI / UNYANYASAJI WA KIJINSIA UNAOWEZESHWA NA TEKNOLOJIA** AU UHALIFU WA KIJINSIA MTANDAONI NI PAMOJA NA MADHARA YA KIMWILI, KINGONO, NA / AU YA KIMHEMKO (AU KISAIKOLOJIA) AMBAO UMEFANYWA MTANDAONI AU KUPITIA MATUMIZI YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (ICT) AMBAO UMEELEKEZWA MWANAMKE KWA SABABU YEYE NI MWANAMKE AU AMBAO HUATHIRI WANAWAKE KWA KIASI KIKUBWA.



JE! NI AINA GANI ZA UDYWM?



- ▶ **UDUKUZI:** UTUMIAJI TEKNOLOJIA KUINGIA BILA YA IDHINI MIFUMO YA VYOMBO VYA MAWASILIANO AU RASILIMALI KWA AJILI YA KUJIPATIA AU KUJIKUSANYIA TAARIFA FULANI ZA KIBINAFSI KUTOKA KWA MTUMIAJI, KUZIBADILISHA AU KUZICHAKACHUA, AU KUMHARIBIA JINA NA KUMKASHIFU MWATHIRIWA NA/ AU MASHIRIKA YA UDYW, K.M. UBADILISHAJI NENOSIRI LA MHSIKA NA UTWAAJI UDHIBITI WA AKAUNTI YAO NA UFIKIAJI WAO.
- ▶ **KUJIFANYA KUWA MTU MWINGINE:** UTUMIAJI TEKNOLOJIA KUGHUSHI UTAMBULISHO NA KUIGA WA MWATHIRIWA KWA AJILI YA KUFIKIA TAARIFA ZAKE BINAFSI, KUMDHALILISHA AU KUMUAIBISHA, KUWASILIANA NAO, AU KUGHUSHI NYARAKA; K.M. UTUMAJI WA BARUA PEPE ZENYE KERO KUTOKA KWA AKAUNTI YA MWATHIRIWA.
- ▶ **UFUATILIAJI / UNYATIAJI KWA NJIA YA MTANDAO:** UTUMIAJI TEKNOLOJIA KUNYATIA NA KUFUATILIA SHUGHULI NA MIENENDO YA MWATHIRIWA IWE KATIKA WAKATI HALISI AU KIHISTORIA; K.M. UFUATILIAJI WA GPS KUPITIA SIMU YA RUNUNU.
- ▶ **UNYANYASAJI WA KIMTANDAO AU UONEVU / UTUMAJI BARUA TAKA/ KEJELI ZA KIJINSIA:** KUTUMIA TEKNOLOJIA KUENDELEA KUWASILIANA, KUMKASIRISHA, KUMTISHIA, NA / AU KUMTIA HOFU MWATHIRIWA; K.M., SIMU / UJUMBE MFUPI USIO NA KIKOMO; KULIMBIKISHA UJUMBE WA SAUTI HADI INASHINDIKANA WENGINE KUWEZA KUACHA UJUMBE.
- ▶ **USAJILI:** KUTUMIA TEKNOLOJIA KUVUTIA WAATHIRIWA WATARAJIWA KATIKA HALI ZA VURUGU; K.V. MACHAPISHO NA MATANGAZO YA UDANGANYIFU (TOVUTI ZA KUCHUMBIANA, FURSA ZA AJIRA); WALANGUZI WANAOTUMIA MAKUNDI SOGOZI/ YA GUMZO, BODI ZA UJUMBE, NA WAVUTI KUWASILIANA / KUTANGAZA.
- ▶ **USAMBAZAJI WENYE NIA MBAYA / PICHA ZA UTUPU / ZA NGONO / PONOGRAFIA ZA KULIPIZA KISASI / UNYANYASAJI UNAOTEGEMEA PICHA / PONOGRAFIA ISIYO YA KIBALI:** KUTUMIA TEKNOLOJIA KUBADILISHA NA KUSAMBAZA TAARIFA ZINAZOHUSIANA NA MWATHIRIWA NA / AU MASHIRIKA YA VAWG; K.M., KUTISHIA AU KUVUJISHA PICHA / VIDEO ZA UTUPU; KUTUMIA TEKNOLOJIA KAMA CHOMBO CHA PROPAGANDA KUENDELEZA UNYANYASAJI DHIDI YA WANAWAKE.

.'PICHA ZA KISASI ZA UTUPU' - MTU ANAPOCHAPISHA AIDHA PICHA ZA UTUPU AU NGONO AU VIDEO ZA MTU MWINGINE MTANDAONI KWA MADHUMUNI YA KUMUAIBISHA NA KUMDHALILISHA, NA HATA KUSABABISHA UHARIBIFU KWA MAISHA HALISI YA MLENGWA (KAMA VILE KUMFANYA KUFUKUZWA KAZI). HII PIA INAJULIKANA KAMA PONOGRAFIA AU PICHA ZA UTUPU / ZA NGONO BILA IDHINI.[]

.'SEXTING' - UCHAPISHAJI WA PICHA NA KUZITUMA HASWA KUPITIA UJUMBE WA MAANDISHI, UNYANYASAJI WA KIMTANDAO, PONOGRAFIA YA WATOTO

JE! UNaweza kufanya nini kuzuia udywm?



▶ **CHUKULIA TAHADHARI TAARIFA UNAZOSHIRIKI MTANDAONI.** PUNGUZA NA UWE MWENYE KUCHAGUA. ZIWEKE AKALINTI ZAKO SALAMA IWEZEKANAVYO. TUMIA NENOSIRI GUMU. USISHIRIKI NENOSIRI LAKO NA MTU YEYOTE. IWAPO UNATAKA KUCHUKUA PICHA ZA UTUPLU, USIJUMUISHE USO WAKO AU KITU CHOCHOTE KINACHOWEZA KUKUTAMBULISHA

▶ ZINGATIA **UPUNGUZAJI WA DATA** YA MAJUKWAA UNAYOTUMIA; KWAMBA YAKUSANYE TU DATA KWA MADHUMUNI MAALUM YANAYOSEMA DATA YAKO INAHITAJIKA KWA HUDUMA NA KWAMBA TAARIFA YALIYO NAYO KUKUHUSU NI SAHIHI, YA KISASA NA IMETOLEWA KWA IDHINI YAKO.

▶ **ZUIA, ONDOA, CHUJA MACHAPISHO** YENYE CHUKI, JUMBE, NA WATU NA RIPOTI / ALAMISHA KWA WASIMAMIZI NA MAJUKWA HAYO YENYEWWE IWAPO UMEELEKEZEWA MATUSI.



▶ **RIPOTI UHALIFU WA MTANDAONI KWA:** MKURUGENZI YA UPELELEZI WA MAKOSA YA JINAI (DCI), S.L.P. BOX 30036 - 00100 NAIROBI. MAZINGIRA HSE, KIAMBU ROAD, MKABALA NA MAKAO MAKUU YA IDARA YA MISITU (FORESTRY DEPARTMENT HEADQUARTERS), KARURA.



▶ **SIMU +254 (0)20 3343312 / +254 (0)20 720** RIPOTI UNYANYASAJI WA MTANDAONI KWA NATIONAL KE-CIRT/CC . TEMBELEA TOVUTI YAO HAPA. NENDA KWA '**REPORT AN INCIDENT**'. BOFYA KWA 'REPORT.' JAZA MAELEZO KUHUSU TUKIO LAKO, UKIJUMUISHA JINA, SHIRIKA LAKO, ANWANI, MADA (INAWEZA KUWA MALIDHUI YA UNYAANYASAJI) NA SEHEMU YA MAONI. BOFYA 'SUBMIT' ILI KUTUMA MALAMISHI YAKO KWA UTAWALA HUSIKA.



KIMEANDIKWA NA RIVA JALIPA | KIMETAFSIRIWA NA BONFACE WITABA | KIMECHORWA NA NZILANI SIMU
WAONGOZA MRADI: LIZ OREMBO, MWARA GICHANGA, NA GRACE GITHAIGA

